

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM



TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (AJIRA YA MKATABA)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam anawatangazia wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wale wenye sifa ya kazi ya Mtangazaji wa Radio na Fundi Sanifu mitambo ya Radio kuomba nafasi za kazi. Kazi hii itakuwa ni ya Mkataba wa miezi mitatu mitatu na mshahara utalipwa kwa mujibu wa Waraka wa Maendeleo ya Utumishi Na. 20 wa Mwaka 2002.

1.0 MTANGAZAJI RADIO DARAJA LA II - NAFASI TATU (3), NGAZI YA MSHAHARA TGS D;

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Mwombaji awe amemaliza Elimu ya Kidato cha IV (Form IV) au Kidato cha sita (Form VI).
- Mwombaji awe na Shahada ya Sanaa, Sayansi au fani nyingine kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.
- Mtangazaji mwenye Shahada au Stashahada ya juu ya Uandishi wa Habari au fani ya “Mass Communication” au Shahada yoyote pamoja na Stashahada ya kawaida ya Uandishi wa Habari kutoka Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
- Mwenye uzoefu na Taaluma ya nyongeza ya Masoko na Utawala (Marketing or Administration atapewa kipaumbele).

1.1 KAZI ZA KUFANYA:-

- Kuandika habari na kutafsiri taarifa na makala mbalimbali za Radio.
- Kuweka kumbukumbu za utekelezaji kazi (Programme records)
- Kuandaa na kurekodi vipindi mbalimbali ndani ya studio.
- Kusaidia kutangaza vipindi na kurekodi ndani na nje ya studio.
- Kusaidia kutafuta wadhamini/Masoko wa vipindi na matangazo.

2.0 MTANGAZAJI RADIO MSAIDIZI - NAFASI TATU (3), NGAZI YA MSHAHARA TGS B;

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Mwombaji awe amemaliza Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au cha Sita (Form VI).
- Mwombaji awe na amefaulu masomo ya Kiingereza, Kiswahili na Sanaa na ambaye amehudhuria mafunzo ya muda wa mwaka mmoja wa kazi ya Utangazaji au Fani ya uandishi wa Habari katika chuo kinachotambuliwa na Serikali.

2.1 KAZI ZA KUFANYA:-

- Hili ni daraja la mafunzo kazini hivyo Mtangazaji Msaidizi katika cheo hicho atafanya kazi chini ya Mtangazaji wa Radio mwenye uzoefu.
- Kusaidia watangazaji kuandaa “Scripts” za muziki na matangazo.
- Kusaidia kutangaza na kurekodi ndani na nje ya studio.
- Kusaidia utafiti wa vipindi vya Radio, Usikivu na Biashara.
- Kusaidia kutafuta wadhamini wa vipindi na Matangazo.

3.0 FUNDI SANIFU MITAMBO WA RADIO-NAFASI MOJA (1), NGAZI YA MSHAHARA TGS C;

SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Mwombaji awe na Elimu ya kidato cha Nne (Form IV).
- Mwombaji awe amehudhuria na kufuzu mafunzo ya miaka mitatu ya Ufundu katika Fani ya Mawasiliano ya Anga, Umeme na Mitambo ya Radio.

3.1 KAZI ZA KUFANYA:-

- Kama fundi sanifu wa Radio pamoja na madaraka zaidi katika kutengeneza na kuendesha mitambo ya Radio.
- Kusaidia kazi za kuendesha Mitambo Studio.
- Kusaidia uendeshaji wa Mitambo ya kurushia matangazo (Transmitters).
- Kufanya kazi za shift-kusaidia kuendesha mitambo studio.

4.0 MASHARTI YA JUMLA:-

- Waombaji wote wawe Raia wa Tanzania wenyе umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi 45.
- Waombaji wote waambatishe nakala za vyeti vya Taaluma, Kidato cha Nne, Cheti cha kuzaliwa na picha mbili (2) za Pasport Size za hivi karibuni, na iandikwe majina yote ya mwombaji kwa nyuma.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na namba za simu za kuaminika na majina matatu ya wadhamini.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **25 Aprili, 2019**.

5.0 MAOMBI YOTE YATUMWE KWA ANUANI IFUATAYO:-

Mkurugenzi wa Jiji,
Halmashauri ya Jiji,
Ukumbi wa Jiji,
S.L.P. 9084,
1 – Barabara ya Morogoro,
11882 – DAR ES SALAAM.

Tangazo hili pia linapatikana kwenye tovuti ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ambayo ni **www.dcc.go.tz**



Sipora J. Liana

MKURUGENZI WA JIJI

HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM